

## **Kwa: Familia za SLPS: Masharti ya COVID ya 2022-2023**

*Tafadhali kumbuka mabadiliko yaliyo hapa chini katika Masharti yetu ya COVID. Ikiwa una maswali au wasiwasi wowote, tafadhali wasiliana na mwalimu mkuu wa shule yako.*

### **Kuripoti Walioambukizwa**

Mwanafunzi yeyote anayetambuliwa kuwa na maambukizi anapaswa kukaa nyumbani kwa **angalau siku 5** kuanzia aliposhuhudia dalili kwa mara ya kwanza au tarehe ya kupimwa kwa mujibu wa [miongozo ya sasa ya kutengwa](#) ya CDC, ikiwa ni pamoja na kurudi shuleni tu wakati hajashuhudia homa kwa saa 24, na **kuvaa barakoa inayotoshea ipasavyo kwa siku 10** baada ya kupatikana kuwa na ugonjwa.

Ili Wilaya ifuatilie viwango vya maambukizi kwenye jengo, tafadhali ripoti pia shuleni ikiwa vipimo vya mwanafunzi vitatambuliwa kuwa na virusi.

**Ingawa kila juhudi itafanywa ili kutoa kazi na kuhakikisha kuwa hawabaki nyuma, hakutakuwa na kipengele cha mtandaoni au cha nyumbani kwenye mtaala wetu wa kawaida mwaka huu. Kwa hivyo, wanafunzi watahesabiwa kuwa hawajahudhuria shule wakati wa kutengwa kutokana na vipimo vyako kutambuliwa kuwa na COVID.**

### **Kuhatarishwa na COVID**

***Tafadhali zingatia mabadiliko haya muhimu katika mwongozo wa 2022-2023:***

Iwapo utarifiwa kwamba umekaribiana na mtu ambaye ana COVID, tofauti na vipimo chanya kama ilivyoonyeshwa hapo juu, ***HUPASWI kuripoti hatari hii kwa Wilaya.*** Wilaya haidumishi tena Idara yoyote ya ndani ya Ufuatiliaji wa Walioambukizwa, wala CDC haipendekezi kufuatilia au kuweka karantini. Iwapo unajua akiyekaribiana na mtoto wako au kuhatarishwa na mtu aliyeambukizwa COVID, fuata [tahadhari za CDC](#), ikiwa ni pamoja na kuvaa barakoa inayotosha ipasavyo kwa siku 10 baada ya mara ya mwisho ya kukaribia mtu aliyeambukizwa, na kufuatilia dalili.

Kwa taarifa yako, unaweza kupata taarifa za sasa kwenye tovuti ya CDC kuhusu masharti ya chanjo za kuimarisha ulinzi ili kupata [taarifa za punde](#) kuhusu chanjo.

### **Dalili za COVID**

Wanafunzi hawapaswi kuwa shuleni wakiwa na mojawapo ya dalili zifuatazo isipokuwa ikiwa imethibitishwa kuwa hawaugui COVID:

Kuhisi baridi/kutetemeka, maumivu ya misuli, maumivu ya koo, kupoteza hisia ya kuonja au kunusa, homa (100.4 au zaidi), au kushindwa kupumua, kukohoa, maumivu ya tumbo, kuhara. Tafadhali rejelea Mchoro wa Uamuzi wa Dalili za Mwanafunzi wa sasa upate maelezo zaidi.

Ikiwa mwanafunzi wako ana dalili na vipimo vyake havijatambuliwa kuwa na COVID, anaweza kuhudhuria shule mradi apate afueni, anaweza kuhusisha dalili hizo na ugonjwa mwingine ambao si COVID, na ikiwa hana homa.

**Masharti haya sharti yazingatiwe hata kama unaamini kuwa dalili za mwanafunzi wako zinatokana na utambuzi mbadala ambao si wa COVID, na hata kama amechanjwa pamoja na taarifa kuhusu chanjo za kuimarisha ulinzi. COVID inaweza kufanana magonjwa yasiyoambukiza kama vile mizio au maambukizo ya kibweta, hivyo basi, COVID haipaswi kudhaniwa katika hali zote.**

Ikiwa mwanafunzi wako ana hali ya matibabu na una dalili zozote zinazofanana na za COVID, tafadhali wasiliana na mwalimu mkuu wa shule na/au mwuguzi. Atatoa mwongozo wa kuwasilisha barua ya daktari inayobainisha kuwa hana maambukizi kwa kuonyesha dalili za mwanafunzi wako hivi kwamba asihitajike kuendelea kupima COVID.

### **Matumizi ya Barakoa**

SLPS inaendelea kupendekeza uvaaji wa barakoa kwa mujibu wa [mapendekezo yote ya uvaaji wa barakoa wa CDC](#), ikiwa ni pamoja na uvaaji wa barakoa kukiwa na viwango vya juu vya maambukizi ya COVID, au ikiwa katika kitengo hatari zaidi. Kama ilivyoelezwa hapo juu, barakoa zinapaswa pia kuvaliwa kwa siku 10 kufuatia (1) kumkaribia mtu aliye na COVID, au (2) vipimo kupatikana kuwa na COVID.

SLPS itafanya juhudi za kupunguza hatari darasani na shuleni kulingana na viwango vya maambukizi katika jengo mahususi. Kwa hivyo, tena, tafadhali hakikisha kuwa unaripoti kwa uongozi wa jengo mwanafunzi wako atathibitishwa kuwa na COVID.

***Sote lazima tutekeleze wajibu wetu ili kudumisha usalama wa mazingira ya shule yetu. Tafadhali zingatia masharti haya na sote tushirikiane kama jumuiya ili kuendelea kufamamishana kuwa salama.***